*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:..........................................................*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03 MAARIFA YA JAMII**

**Muda: 1: 30** **Jumatano, 25 Oktoba, 2023 Mchana.**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina jumla ya maswali **manne (04).**
2. Jibu Maswali yote.
3. Andika Namba yako ya Upimaji katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| **KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU** | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MPIMAJI** |
| **1** | | |
| **2** | | |
| **3** | | |
| **4** | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:..........................................................*

## SEHEMU A (ALAMA 26)

1. Jibu kipengele (i) –(vii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kisha andika katika kisanduku uliyopewa:

i) Yapi ni mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania?

A. Mahindi, chai na kahawa.
B. Pamba, chai na kahawa
C. Ndizi, kahawa na pamba
D. Mihugo, mpunga na tumbaku

ii) Ipi nifaida ya utalii nchini Tanzania?

A. Kuiga mila na desturi za wageni
B. Kupata fedha za kigeni]
C. Kuongezeka kwa mazao ya misitu
D. Kuongezeka kwa wanyama pori.

iii) Madini ya almasi yana matumizi gani?

A. Kukatia vioo
B. Chanzo cha nishati ya joto
C. Kukatia chuma
D. Kuzalisha umeme
E.

iv) Mbuga ipi ni kubwa kuliko yote nchini Tanzania?

A. Ruaha
B. Ngorngoro
C. Mikumi
D. Serengeti



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

v) Bainisha wanyama wanaofungwa kati ya wafuatao:

A. Simba, ng'ombe na kondoo
B. Pundamilia,kondoo na chui
C. Twiga, kondoo na mbuzi
D. Mbwa , kondoo na mbuzi.

vi) Ipi ni njia sahihi ya kutunza misitu?

A. Kuchoma miti ili kupunguza msongamano
B. Kuzalisha mkaa ili kuongeza kipato
C. Kupanda miti mingine baada ya kuta ya awali
D. Kujenga maeneo ya misitu ili kupata hewa safi

vii) Ni madini yapi hutumika kutengeza saruji

A. Chuma
B. Chokaa
C. Fosfeti
D. Chumvi

viii) Kwanini kilimo ni uti wa mgongo  kwa uchumi wa Tanzania?

A. Huvutia watalii wengi
B. Watu wengi wameajiriwa kwenye kilimo
C. Watu wengi huishi mashambani
D. Wawekezaji wengi wamewekeza kwenye kilimo



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Jibu kipengele cha (i)-(vi) kwa kuoanisha mchango wa mashujaa wa Tanzania katika Fungu A na majina yao katika Fungu B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopew:

<table>
<tr><th>No.</th><th>Fungu A</th><th>Herufi</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>(i)</td><td>Aliwaongoza waafrika kuoinga uvamizi wa wajerumani katika eneo la kilwa kivinje 1890</td><td>[ ]</td><td rowspan="6">A. Chief Machemba<br>B. John P. Magufuli<br>C. Abushiri Bin Sultan<br>D. Benjamin w. Mkapa<br>E. Bwana Heri<br>F. Ali H. Mwinyi<br>G. Julius K. Nyerere<br>H. Hasan Bin Omar Makunganya</td></tr>
<tr><td>(ii)</td><td>Alianzisha sera ya soko huria</td><td>[ ]</td></tr>
<tr><td>(iii)</td><td>Aliwaongoza wazigua kupinga uvamizi wa kierumani katika eneo la Tanga mwaka 1890.</td><td>[ ]</td></tr>
<tr><td>(iv)</td><td>Alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote muanzia darasa la awali hadi kidato cha nne</td><td>[ ]</td></tr>
<tr><td>(v)</td><td>Aliwaongoza wayao wa masasi na tunduru kupigana na wajerumani mwaka 1890</td><td>[ ]</td></tr>
<tr><td>(vi)</td><td>Alianzisha mfumo wa ubinafssgaji.</td><td>[ ]</td></tr>
</table>



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Shule yetu ina mazingira safi. Mazingira machafu ni maficho ya wadudu na anyama hatarishi kama inzi, mbu, panya na nyoka. Kati ya viumbe hao, nyoka ni hatari zaidi kwa kuwa sumu yake ina madhara makubwa kwa binadamu na wanyama wengine. Ni muhimu kuishi katika mazingira safi.

Mazingira safi hupunguza kuenea kwa magonjwa mbalimbali kama malaria na kipindupindu Malaria huenezwa na mbu wanaoishi katika majani marefu na maji yaliyotuama. Kipindupindu husababishwa na inzi wanaoishi kwenye majani marefu. Magonjwa hayo yanaweza kuepukika kwa kufyeka nyasi na kufukia mashimo yenye maji ili maji yasituame. Mazingira safi pia hutusaidia kupata hewa safi ya oksijeni. Ili kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanaendelea kuwa safi, ni lazima tufanye usafi wa mazingira kila siku kwa kutumia jembe na fyekeo.

**Maswali:**

a) Kwanini ni muhimu kuishi katika mazingira safi?

_____________________________________________________

b) Ni kiumbe hai kipi amcho kina sumu ambaco huweza kudhuru watu na viumbe wengine?_______________________________________

c) Kwa kuzingatia kifungu cha habari , taja kifaa kimoja kinachotumika kufanya usafi.____________________________________________

d) Ni ugonjwa gani unaweza kuepukwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama.__________________________________________

e) Ni mdudu yupi anaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa wa kipindipindu?______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

f) Kutokana habari uliyosoma, wadudu na wanyama hatarishi hupatikana wapi?

__________________________________________________

g) Ni namna gani tunaweza kuwa na mazingira safi?

__________________________________________________

4. Chora alama za ramani kuonesha vitu vifuatavyo:

| **Aina ya Kitu** | **Alama ya Ramadhani** |
|---|---|
| (a) Mlima | |
| (b) Daraja | |
| (c) Reli | |
| (d) Kiwanja cha ndege | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org